



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA  
BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI ZA GHALA



**TANGAZO KWA WAENDESHA GHALA WOTE  
{MABADILIKO MADOGO YA RATIBA YA MAFUNZO}**

Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) ni taasisi chini ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara iliyoundwa kwa Sheria Namba 10 ya Mwaka 2005 na marekebisho yake chini ya Sheria Namba 4 Sura ya 339 R.E. 2016. Bodi imepewa majukumu chini ya Kifungu 5 (a-j) cha Sheria hiyo ikiwemo kutoa leseni kwa Waendesa Ghala, Meneja Dhamana na Wakaguzi wa Ghala.

Kufuatia tangazo la Awali ambapo Bodi ilikuwa imeandaa mafunzo ya wafanyakazi wa ghala kuanzia tarehe **24 hadi 26 Septemba 2022** katika **Ukumbi wa Chuo cha Kilimo Mtwara (MATI)** mkoani Mtwara. **Tarehe za mafunzo haya haitabadilika.**

Aidha, mafunzo kwa **Wakurugenzi** na **Mameneja** wote wa kampuni zinazotarajia kuendesa ghala msimu wa korosho 2022/2023 sasa yatafanyika siku **ya ufunguzi wa mafunzo tarehe 24 Septemba 2022 kuanzia saa tatu kamili asubuhi mpaka saa sita kamili mchana** na baada ya hapo mafunzo kwa watumishi wengine wote yataendelea kama ilivyokuwa imepangwa awali.

Mgeni Rasmi katika Ufunguzi wa mafunzo hayo anatarajiwa kuwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara na pia katika siku hiyo Wakurugenzi wa Taasisi wadau wa Mfumo wa Stakabadhi za ghala ikiwa ni Pamoja na Bodi ya Korosho Tanzania (CBT), Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mkurugenzi wa Mazao, Wizara ya Kilimo watahuduria.

Tunaomba radhi kwa usumbufu wowote utakaojitokeza.

Imetolewa,

**Kaimu Mkurugenzi Mtendaji**  
16 Septemba 2022